**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO**
**YA UFUNDI STADI**

**CHUO CHA MKOA CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA MBEYA**

# MAELEZO MUHIMU YA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA 2025

## MAELEZO HAYA YASOMWE KWA UMAKINI NA MZAZI/MLEZI WA MWANACHUO

1. Wanachuo wote zingatieni kufika siku hiyo ya kufungua chuo kama ilivyoelezwa kwenye **barua ya kujiunga na chuo** kabla ya saa 12:00 jioni. Hatutapokea mwanachuo siku zisizokuwa za kazi na hupaswi kufika kabla ya tarehe ya kufungua chuo.
2. **Tafadhali: ufikapo chuoni, fika na cheti chako halisi pamoja na kivuli cha kidato cha nne ama cheti cha darasa la saba au taarifa rasmi ya mkuu wa shule ya msingi uliyo hitimu darasa la saba.**
3. Kwa kila mwanachuo alie na umri wa miaka 18 au zaidi anapaswa kuwa na **namba ya nida** na kuiwasilisha chuoni siku ya kuripoti.
4. Kama unacho kitambulisho cha **BIMA** ya afya Ulichopewa kazini au kupitia mzazi/mlezi hupaswi kulipa fedha ya Bima ya afya. Uje na kitambulisho chako (**MUHIMU:** BIMA INAYOHITAJIKA NI **NHIF** TU).

5. Gharama za wanachuo waliochaguliwa kukaa **BWENI** ni kama ifuatavyo :
   - Suruali mbili za dark blue Tsh. 45,000/=
   - Ovaroli moja rangi ya dark blue kwa wanachuo wote [isipokuwa fani ya UPISHI, USHONAJI NA UHAZILI NA KOMPYUTA ambao watavaa ovakoti] - Tsh. 28,000/=
   - Fulana ya VETA Tsh. 17,000/=
   - Nembo mbili za VETA Tsh. 4,000/=
   - Fedha za michezo Tsh. 18,000/=
   - Fedha za kitambulisho Tsh. 6,000/=
   - Fedha za tahadhari Tsh. 10,000/=
   - Bima ya Matibabu Tsh. 50,400/=
   - Ada ya mtihani wa Stadi za maisha 25,000/=
   - Ada ya mafunzo kwa mwanachuo wa **BWENI** kwa mwaka ni Tsh. 120,000

- **JUMLA YA FEDHA YOTE KWA MWANACHUO WA BWENI NI TSH 323,400/= KWA MWAKA**
- **MUHULA WA KWANZA KWA MWANACHUO WA BWENI ALIPE TSH. 263,400/= TU. ILIPWE KABLA YA KUANZA MASOMO MWEZI JANUARI 2025.**
- **MUHULA WA PILI KWA MWANACHUO WA BWENI ALIPE TSH. 60,000/= TU. ITALIPWA MWEZI JULAI 2025.**

6. Gharama za mwanachuo aliyechaguliwa kusoma akiwa anatokea **NYUMBANI ( KUTWA)** ni kama ifuatavyo :
   - Suruali mbili za dark blue Tsh. 45,000/=
   - Ovaroli moja rangi ya dark blue kwa wanachuo wote [isipokuwa fani ya UPISHI, USHONAJI NA UHAZILI NA KOMPYUTA ambao watavaa ovakoti] - Tsh. 28,000/=
   - Fulana ya VETA Tsh. 17,000/=
   - Nembo mbili za VETA Tsh. 4,000/=
   - Fedha za michezo Tsh. 18,000/=
   - Fedha za kitambulisho Tsh. 6,000/=
   - Fedha za tahadhari Tsh. 10,000/=
   - Bima ya Matibabu Tsh. 50,400/=
   - Ada ya mtihani wa Stadi za maisha 25,000/=
   - Ada ya mafunzo kwa mwanachuo wa **KUTWA** kwa mwaka ni Tsh. 60,000/=

- **JUMLA YA FEDHA YOTE KWA MWANACHUO WA KUTWA NI TSH. 263,400/= KWA MWAKA.**
- **MUHULA WA KWANZA KWA MWANACHUO WA KUTWA ALIPE TSH. 233,400/= TU. ILIPWE KABLA YA KUANZA MASOMO MWEZI JANUARI 2025.**
- **MUHULA WA PILI KWA MWANACHUO WA KUTWA ALIPE TSH. 30,000/= TU. ITALIPWA MWEZI JULAI 2025.**

**WANACHUO WOTE ZINGATIENI**

- Ada ya mtihani (25,000/=) **inalipwa pekeake** kwa *control number* inayopatikana ofisi ya msajili.
- Hela ya bima ya afya (50,400/=) **inalipwa pekeake** kwa *control number* inayopatikana ofisi ya msajili.
- Kabla ya kulipa ada na michango mingine, fika chuoni upewe utaratibu wa namna ya kulipia ikiwa ni pamoja na namba ya malipo ya serikali (control number) yakulipia ada, bima ya afya, mtihani na namba ya akaunti ya kulipia michango mbalimbali.
- **Hatupokei fedha taslimu.**
- Baada ya kulipa fedha bank wanachuo wote waje na **RISITI YA BENKI** iliyoandikwa jina la mwanachuo kisha kuiwasilisha ofisi ya uhasibu ili wabadilishiwe na kupewa **RISITI YA VETA**.
- Kila mwanafunzi apeleke RISITI YA VETA katika ofisi ya msajili ili irekodiwe na baada ya hapo **NI JUKUMU LA MWANAFUNZI KUTUNZA RISITI ZAKE ZOTE ZA MALIPO KWA MUDA WOTE WA MAFUNZO.**
- Lipa fedha kiasi ulichoagizwa tu. Ada ikishalipwa hairudishwi.
- Vifaa vinavyotakiwa kwa kila mwanachuo kwa ajili ya fani yake vitaagizwa na mwalimu punde masomo kwa vitendo yatakapoanza.
- **MWANACHUO HURUHUSIWI KUINGIA DARASANI BILA KIBALI KUTOKA OFISI YA MSAJILI.**

7. Unatakiwa kununua vifaa vifuatavyo kwa matumizi yako binafsi :-
    - Mashati mawili meupe (mikono mifupi ya tetron).
    - Sweta moja la bluu iliyokolea.
    - Mkanda wa ngozi wenye rangi nyeusi.
    - Jozi moja ya viatu vyeusi vya ngozi, vya kufunga kamba visigino vifupi.
    - Viatu vya karakana aina ya (safety boots) rangi nyeusi kwa ajili ya usalama utakapokuwa karakana.
    - Vifaa vya hesabu (mathematical set).
    - Daftari kubwa (11).
    - Kalamu na penseli za kuchorea na pen za kuandikia kwa wote.
    - Waliochaguliwa fani ya Upishi na Huduma za Hoteli (FOOD PRODUCTION) waje na apron nyeupe, kofia nyeupe zenye malighafi ya pamba (isiwe tetron) kwa ajili ya kuvaa kichwani wakati wa mafunzo kwa vitendo
    - Wanachuo wote wa bweni watapaswa kuja na godoro la futi (3 x 6), mto wa kulalia, shuka 2 za rangi ya bluu na foronya zake, blanket, chandarua, bakuli, sahani, kikombe, kijiko, ndoo kwa matumizi binafsi, beseni la kufulia, nguo za kujikinga na baridi utakapokuwa bwenini, pamoja na vifaa vya usafi binafsi. **Tracksuits** (Dark Blue colour) kwa wanachuo wa kiume na tracksuits (Dark Brown [Damu ya Mzee]) kwa wanachuo wa kike.
8. Wote mnapaswa kuja na kwanja moja.
9. Wote mnapaswa kuja na Karatasi nyeupe (A4 ) ream moja.
10. Mwanachuo unatakiwa kujaza fomu ya uchunguzi wa matibabu (medical examination form) pamoja na fomu ya kukubali nafasi ya mafunzo ya ufundi stadi.
11. Mwanachuo hatapokelewa chuoni iwapo atafika bila kutekeleza vifungu vyote vilivyotajwa hapo juu.
12. Sheria za chuo zimeambatanishwa, mwanafunzi na mzazi mnatakiwa kusoma kwa makini. Taratibu zingine za chuo zitatolewa utakapofika Chuoni.
13. Mwanachuo unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo

Wako,
**CHUO CHA MKOA CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA – MBEYA**

**Eng Hassan Kalima**
**MKUU WA CHUO**

*VET MED FORM – 1E*

# VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

## MEDICAL EXAMINATION FORM

Date …………………………………………

The Medical Officer

………………………………………………….

………………………………………………….

………………………………………………….

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION:**

Name of trainee ……………………………………………………………..

Please Examine the above named trainee to his/her fitness to undergo training and subsequently work as a/an ……………………………………………………………………………………….

Eyesight ……………………………………………………………………………

Hearing …………………………………………………………………………….

Asthma …………………………………………………………………………….

Other serious diseases ………………………………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE:**

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for training as above.

Date……………………………………………..      Designation …………………………………

Signature and Official stamp ………………………………………………

*VET DECL FORM -1F*

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

**a) MWANACHUO**

Mimi ………………………………………………………………………………………….. ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

Namba za simu ya mwanachuo 1:……………………………… 2:………………………………

Saini ya mwanachuo ……………………………… Tarehe……………………………………

**b) MDHAMINI**

Mimi…………………………………………………………………………….ambaye ni………………………………………………… wa mtajwa hapo juu, nathibitisha kuwa nitamdhamini na nitamlipia gharama zote za mafunzo ikiwa ni ada na gharama nyingine kama ilivyoelekezwa katika maelezo ya kujiunga na chuo na nauli ya kwenda chuoni na kurudi nyumbani wakati wote wa likizo na baada ya mafunzo.

Namba za simu ya mdhamini 1:…………………………… 2:………………………………

Saini ya mdhamini ……………………………………… Tarehe……………………………………

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**CHUO CHA MKOA CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA MBEYA**

---

**SHERIA ZA CHUO KWA WANACHUO WOTE**

**ILI KUFANIKISHA MAFUNZO YA AWALI YA UFUNDI KWA KILA MWANACHUO ANATAKIWA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO:**

Kwa muda wote Mwanachuo unapokuwepo chuoni unatakiwa kufuata taratibu na sheria za chuo. Kutokufanya hivyo kunaweza kupelekea hatua kali za kinidhamu kuchukuliwa dhidi yako. Zifuatazo ni taratibu na sheria za chuo:-

1. **MAHUDHURIO**

(a) Kila mwanachuo anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1.30 asubuhi. Hii ina maana ifikapo saa 1.30 asubuhi wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni.

(b) Mwanachuo hatakiwi kutoka chuoni kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote kwa sababu ya msiba, kuuguliwa au kuugua ni lazima apate kibali cha Mkuu wa chuo.

(c) Mahudhurio chini ya 85% mwanachuo hataruhusiwa kufanya mtihani.

(d) **Ni Marufuku kwa mwanachuo kuingia au kutumia simu ya mkononi sehemu yoyote inayohusiana na mafunzo ikiwa ni darasani au kwenye karakana**.

2. **MAVAZI NA USAFI WA MWILI**

(a) Mwanachuo unatakiwa kuvaa sare ya chuo ambayo ni suruali ya “blue” yenye vipimo vilivyothibitishwa na chuo wakati wote unapokuwa katika mazingira ya chuo. Shati jeupe la mikono mifupi lenye nembo ya VETA lililo chomekewa vizuri ndani ya suruali. Mkanda wa ngozi wa rangi nyeusi. **Mwanachuo atakayevaa sare ya chuo isiyokidhi vipimo atalazimika kushona /kununua nyingine**.

(b) Sare ya chuo itavaliwa wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Ovaroli litavaliwa wakati wa vipindi vya mazoezi kwa vitendo.

(c) Viatu vyenye visigino virefu, kandambili au viatu vya wazi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni wakati wa mafunzo.

(d) Hairuhusiwi kuvaa mapambo ya aina yoyote ile mfano hereni, pete, bangili, mkufu kwa kipindi chote cha mafunzo.

(e) Mwanachuo huruhusiwi: kupaka rangi za midomo, kuweka dawa/rangi za nywele, manukato yanayotoa harufu kali, kufuga kucha au kuzipaka rangi, kuvaa bangili, hereni, mkufu, au urembo wowote.

(f) Nywele kwa wavulana:
Zikatwe ziwe fupi na isiwe kipara. Hairuhusiwi kunyoa mitindo mingine na kufuga **Sharubu** **au** **Ndevu**.

(g) Nywele kwa wasichana:
Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma **(twende kilioni).** **Hairuhusiwi kunyoa au kusuka mitindo nje ya iliyoruhusiwa.**

**USAFI WA MAZINGIRA YA CHUO**

i) Mwanachuo unatakiwa kutunza usafi wa mazingira ya chuo ikiwa ni pamoja na kutoandika katika kuta za majengo na kutokukatisha katika sehemu isiyoruhusiwa.
ii) Mwanachuo huruhusiwi kubandika tangazo lolote katika kuta na mbao za matangazo, wala kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.
iii) Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake, hairuhusiwi kupeleka meza au viti mabwenini.

3. **WIZI, UPOTEVU NA UHARIBIFU WA VIFAA**:

(a) Vitendo vyovyote vinavyohusisha wizi ni kosa la jinai.
(b) Ukipoteza au kuharibu kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa au ukakinunue kifaa chenyewe.
(c) Hairuhusiwi mwanachuo kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo bila idhini ya mkuu wa chuo.
(d) Mwanachuo atapekuliwa au kukaguliwa wakati wa kutoka au kuingia karakana na getini.

4. **UGOMVI**

Kupiga, kupigana na kushambuliana kwa maneno ni makosa ya jinai.

5. **ULEVI**

Mwanachuo haruhusiwi kulewa au kuonekana katika sehemu za vileo, kuvuta bangi au kutumia madawa ya kulevya.

6. **MAPENZI:**

(a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya wanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanachuo hairuhusiwi kabisa.
(b) Mwanachuo yeyote haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi wafanyakazi wa chuo bila kibali au ruhusa.

7. **MIGOMO:**

Kushiriki, kushawishi au kuchochea migomo ni kosa la jinai.

**JEDWALI LA MAKOSA MBALIMBALI NA ADHABU ZAKE**

| Na. | MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA CHUO | MAKOSA YANAWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA MASOMO/ KUNYANG'ANYWA NAFASI YA BWENI | MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUPELEKEA KUPEWA ADHABU |
|---|---|---|---|
| | a) Wizi, rushwa na utapeli.<br>b) Ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji bangi.<br>c) Kupiga au kupigana.<br>d) Ubakaji na ushoga chuoni.<br>e) Kudharau bendera ya Taifa.<br>f) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo, kuvuruga amani na usalama wa Chuo na watu.<br>g) Kufanya jaribio lolote la kujiua/kuua.<br>h) Kushiriki vitendo vya ugaidi.<br>i) Utoro uliokithiri.<br>j) Kumlaza mgeni bwenini.<br>k) Kupika chakula /kutumia "heater" bwenini. | a) Kukataa adhabu halali.<br>b) Kuharibu mali ya chuo.<br>c) Uasherati<br>d) Kutofanya mitihani/mazoezi bila sababu.<br>e) Kufanya biashara na kujihusisha na siasa chuoni.<br>f) Kuingia na mgeni/kumkaribisha mgeni bwenini.<br>g) Kutumia vifaa visivyoruhusiwa bwenini.<br>h) Kulala nje ya chuo bila ruhusa ya Mkuu wa Chuo.<br>i) Kutumia lugha ya matusi.<br>j) Kutovaa sare ya chuo awapo nje ya chuo. | a) Kuingia maeneo yasiyoruhusiwa.<br>b) Kuingia na kifaa chochote kile kinacho fanana na vilivyoko ndani ya chuo bila ruhusa.<br>c) Kupeleka meza au viti bwenini.<br>d) Kubandika tangazo lolote katika kuta na mbao za matangazo, kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.<br>e) Kutotunza usafi wa mazingira ya chuo.<br>f) Kukatisha katika sehemu isiyoruhusiwa.<br>g) Kutozingatia usafi wa mwili.<br>h) Kutoka nje ya chuo bila ruhusa.<br>i) Kuchelewa kuripoti chuoni kabla ya saa 1.30 asubuhi<br>j) Kupoteza kifaa cha chuo. |